

Photo by Emediong Umoh on Unsplash

# Uelewa kuhusu sheria za vitendo vya kashfa Tanzania

Julai 2025

TrustLaw | Thomson Reuters Foundation

IDEAL LAW GROUP
LEGAL PARTNER IN BUSINESS

WatchAfrica



SHUTTERSTOCK/Wellphoto

# Utangulizi

Sheria za kashfa zikitumika kwa usahihi, zinatarajiwa kulinda watu binafsi na watu maalumu dhidi ya taarifa za uongo zinazoweza kuharibu sifa yao. Ingawaje, sheria za madai na za jinai za kashfa zikitumika vibaya zinaweza kuzuia mijadala ya wazi ya umma.

Mwongozo huu unalenga kuwapatia waandishi wa habari uelewa kwa vitendo kuhusu sheria za kashfa/kuharibu sifa ya mtu pamoja na hatua wanazoweza kuchukua ili kupunguza uwezekano wa kuwajibika kisheria kulingana na sheria hizo nchini Tanzania. Uelewa huu utawawezesha waandishi wa habari kufahamu haki na wajibu wao wa kisheria na kuwawezesha kuendelea kutoa taarifa za masuala yenye umuhimu kwa masilahi ya umma. Mwongozo huu unajumuisha mawanda ya sheria za kashfa, mwenendo wa mashauri ya jinai na madai mahakamani, utetezi dhidi ya madai ya kashfa, adhabu zinazotolewa dhidi ya kashfa na hatua za tahadhari zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza hatari ya kuwajibika kisheria.



REUTERS/Thierry Gouegnon

# 1. Mawanda ya kashfa

## Kashfa ni nini?

Kwa ujumla, kashfa inaweza kufafanuliwa kuwa ni kauli ya uongo inayotolewa na mtu, iwe kwa mdomo au kwa maandishi, ambayo husababisha madhara kwa kuharibu sifa ya mtu mwingine. Nchini Tanzania, vitendo vya kashfa vinasimamiwa na kanuni za kawaida za kisheria (kuhukumu kesi kwa kuzingatia maamuzi ya kesi zilizokwishaamuliwa mahakamani), pamoja na sheria za kimila (jumla ya matendo, imani na desturi zinazokubalika kuwa ni kanuni za mwenendo katika jamii).

Nchini Tanzania, kashfa inafafanuliwa kuwa ni uchapishaji wowote ambao una uwezekano wa kumweka mtu (aliye hai au aliyefariki) katika hali ya kuchukiwa, kudharauliwa au kubezwa.[1] Uchapishaji unajumuisha:

(a) Uchapaji.
(b) Maandiko.
(c) Uchoraji.
(d) Kuchonga sanamu au kinyago cha dhihaka.
(e) Njia nyingine kama vile maonesho, usomaji, usimulizi, maelezo, au usambazaji wa taarifa.[2]

1 Kifungu cha 35(1) na 35(2) cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016.
2 Kifungu cha 36 cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016.

# Ni mambo gani yanabainisha kashfa ya jinai na kashfa ya madai?

Kuna tofauti kuu mbili kati ya kashfa za madai na za jinai:

**(a)** utambulisho wa upande unaowasilisha shauri; na
**(b)** kiwango cha uthibitisho kinachotakiwa ili kuthibitisha madai.

Katika mashauri ya madai, upande unaodai kukashfiwa (mdai) utawasilisha shauri mahakamani ambalo ni lazima lithibitishwe kwa kipimo cha welekeo wa uwezekano (kiwango cha uthibitisho kinachohitajika katika shauri la madai). Hii inamaanisha kuwa ushahidi uliotolewa una uwezekano mkubwa wa kuwa kweli kuliko uongo. Kwa upande wa kosa la jinai, ni Mkurugenzi Mwendesha Mashtaka wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka anayewasilisha kesi hiyo na ni lazima athibitishe kila kipengele cha kosa bila kuonesha shaka yoyote. Hii inamaanisha kuwa upo ushahidi wa kiwango cha juu katika kesi ya jinai ikilinganishwa na ule wa kesi za madai. Kesi za jinai kwa kawaida huadhibiwa kwa kutoa faini, kifungo au vyote viwili kwa pamoja. Kwa upande mwingine, kesi ya madai ya kashfa/kumkashfu mtu, huadhibiwa kwa kulipa fidia ya fedha kwa mdai kama ilivyoamriwa na mahakama.

Ijapokuwa hakuna jinai ya kashfa katika Kanuni za Adhabu baada ya vifungu vya 187-194 kufutwa, bado uchapishaji wa taarifa za uongo zinazomkashfu mtu, kumtishia, kumtukana au kupotosha umma ni kosa la jinai.[3] Hata hivyo, kifungu hicho kinarejelea taarifa zilizochapishwa kupitia "mfumo wa kompyuta" na haijabainika wazi kama uchapishaji wa aina nyingine unaweza kuchukuliwa kuwa ni kosa la jinai.

# Ni katika mazingira gani ninaweza kufunguliwa kesi ya madai ya kashfa?

Unaweza kufunguliwa kesi ya madai kwa kuharibu sifa ya mtu yeyote binafsi au taasisi (kupitia wawakilishi wake kama wakurugenzi wa kampuni) wanaoamini kuwa sifa yao imeharibiwa kwa kauli yako inayodaiwa kuwa ni kashfa).

Ili mtu aweze kufanikisha kuanzisha shauri dhidi yako kwa sababu ya madai ya kumkashfu ni lazima athibitishe kuwa kauli iliyofanya washtaki:

**(a)** ilikuwa ya uongo;
**(b)** ilikuwa ni kashfa;
**(c)** ilichapishwa kwa mtu mwingine;
**(d)** taarifa hiyo ilimhusu moja kwa moja mtu binafsi au taasisi inayodai kuathirika na kashfa hiyo.

Iwapo mahakama itathibitisha kuwa kauli inayolalamikiwa ilikuwa kashfa, utawajibika kisheria, isipokuwa kama utajitetea kwa kuwasilisha utetezi wako kama inavyoelezwa hapa chini.

3 Kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya 2015.

# Je, ni mazingira gani ninaweza kushtakiwa kwa kuchapisha taarifa za uongo zinazoweza kushusha/kuharibu sifa ya mtu?

Unaweza kushtakiwa iwapo ulichapisha kwa makusudi taarifa za uongo ambazo zina uwezekano wa kuathiri au kuharibu sifa ya mtu.[4] Ili uhukumiwe kwa kosa hilo la jinai, upande wa mashtaka lazima uthibitishe kuwapo kwa dhamira ya kufanya jinai na chapisho halisi la madai ya uongo. Mashtaka lazima yaoneshe, bila shaka yoyote kwamba ulijua kuwa taarifa hiyo haikuwa ya kweli na uliichapisha kwa lengo la kuharibu sifa ya mtu, kwa kuwapo kwa dhamira ya kufanya jinai na chapisho halisi la madai ya uongo vyote kwa pamoja.

# Je, sheria inatambua matamshi ya chuki kama kosa la jinai?

Matamshi ya chuki ni kosa la jinai nchini Tanzania. Matamshi ya chuki hurejelea maelezo ya maneno, hotuba au picha au namna nyingine yoyote, ambayo inaadhiri, inakashifu, au kudharau mtu au kundi la watu kutokana na kigezo cha rangi, kabila, dini au ulemavu.[5] Adhabu ya kuwa na hatia ya kufanya kosa la matamshi ya chuki ni faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania milioni tano (Tshs. 5,000,000) au kifungo kisichopungua mwaka mmoja, au vyote viwili kwa pamoja.

Aidha, ni kosa la jinai kuchapisha maudhui ya kibaguzi na ya chuki dhidi ya wageni. Hii inajumuisha maudhui yoyote yanayochochea, kuhamasisha au kuendeleza chuki, ubaguzi au vurugu dhidi ya mtu au kundi la watu kwa misingi ya rangi, asili, ukoo, taifa, kabila au dini.[6] Ikitokea mtu amehukumiwa kwa kosa la kuchapisha maudhui ya kibaguzi au ya chuki dhidi ya wageni, anaweza kutozwa faini isiyopungua Shilingi milioni tatu (Tshs. 3,000,000) au kifungo kisichopungua mwaka mmoja, au vyote viwili kwa pamoja.

# Je utapata hasara zipi kwa kupatikana na hatia ya kuchapisha taarifa za uongo?

Kuchapisha taarifa za uongo kunaweza kukusababishia adhabu ya kutozwa faini ya hadi Shilingi za Kitanzania milioni tano (Tshs. 5,000,000), au kifungo kisichopungua miaka mitatu, au vyote viwili kwa pamoja.[7]

4 Kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya 2015.
5 Kanuni ya 3 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni) za 2020.
6 Kifungu cha Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya 2015.
7 Kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya 2015.

# Ni adhabu zipi zinazoweza kutolewa endapo utapatikana na hatia ya madai ya kukashfu mtu?

Iwapo utashtakiwa na mdai kwa kosa la kumkashfu/kuharibu sifa yake, mahakama inaweza kutoa amri ya:

(a) **Kulipa fidia:** Iwapo taarifa za kashfa zimeshachapishwa na mtu binafsi/au taasisi inathibitisha madai yake kwa kutoa ushahidi dhidi ya mwandishi wa habari, basi mtu/taasisi ina haki ya kulipwa fidia ya fedha kutokana na madhara ya kuharibiwa sifa zake.

(b) **Kukanusha na/au kuomba msamaha:** Mahakama inaweza kuamuru kuwa makala au taarifa yenye kashfa iondolewe au kukanushwa, na kwamba msemaji au mwandishi atoe pole au aombe msamaha rasmi, iwapo mdai ameomba hivyo na baada ya mahakama kujiridhisha kuhusiana na ukweli wa shauri.

# Mifano ya mashauri ya kesi za kashfa

## Kashfa za Madai

- Benard Kamilius Membe dhidi ya Cyprian Majura Musiba na Wengine[8]

Katika shauri hili, mlalamikaji, ambaye ni Waziri wa Zamani wa Serikali ya Tanzania na mwanasiasa, aliwashtaki washtakiwa wakiwamo Musiba na *Gazeti la Tanzanite* kwa kuchapisha mfululizo wa makala yenye kauli zenye kashfa zilizoharibu sifa yake. Machapisho hayo yalimshutumu kwa uongo kuwa Membe alijihusisha na vitendo vya wizi wa kura, utakatishaji wa fedha, na kuwa tishio kwa usalama wa taifa, madai yaliyosababisha madhara kwa mtu binafsi, kitaaluma na kifedha. Mahakama ilibaini kuwa washtakiwa wana hatia ya kumkashfu Membe na kuwaamuru wamlipe fidia ya jumla na kuwa mfano, na pia ikatoa zuio dhidi ya uendelezaji wa machapisho mengine yenye kashfa dhidi ya Membe.

Kesi hii ilisisitiza mambo ya msingi yanayopaswa kuthibitishwa katika kesi ya kumkashfu mtu/kuharibu sifa ya mtu, ikiwa ni pamoja na kuthibitisha kuwa taarifa ilikuwa ya uongo, ilikuwa ni kashfa, ilichapishwa kwa ajili ya mtu mwingine, na inamrejelea mdai. Vilevile, shauri linaelezea ukweli kwamba, ulipaji wa fidia katika shauri la kumkashifu mtu ni jambo la hiari. Katika shauri hilo, mahakama ilimwamuru mshtakiwa ambaye ni mwandishi wa habari kulipa fidia ya Shilingi Bilioni Saba (Tshs. 7,000,000,000) kwa mlalamikaji.

8 Kesi ya Madai Na. 220 ya 2018.

### Augustino Ellas Mdachi dhidi ya Ramadhan Omary Ngaleba[9]

Katika kesi hii, mdaiwa alikata rufaa kupinga uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi uliomkuta na hatia ya kumkashifu mlalamikaji. Tukio lililotajwa lilitokea tarehe 22 Julai 2016, katika Mtaa wa Kidimu, Kata ya Pangani, Halmashauri ya Mji Kibaha. Ngaleba alikuwa akisimamia malori yake ambayo husafirisha mchanga kutoka shambani kwake, aliposimamishwa na Mdachi, Diwani wa Kata ya Pangani, aliyekuwa ameambatana na maofisa wengine wawili. Mdachi alidaiwa kutoa maneno ya kashfa dhidi ya Ngaleba kwa kumtuhumu kuvuna mchanga bila leseni. Mahakama Kuu iliamua kuwa madai kuhusu ukosefu wa leseni yalikuwa ya kweli na hayakuwa ya kashfa kwa kuwa mlalamikaji hakuwa na leseni ya uchimbaji wa mchanga. Aidha, mahakama ilibaini kuwa haikuwa na ushahidi wa mashtaka ya nia ovu wala madhara yaliyothibitishwa. Mahakama pia ilieleza kuwa jukumu la kuthibitisha ukweli wa madai ni la mpinga rufaa, na kwamba Mdachi alitimiza hilo kwa ushahidi kwamba Ngaleba hakuwa na leseni.

### Mch. Isack Richard dhidi ya Askofu Solomon Rukumaye na Wengine Watatu[10]

Mchungaji Isack Richard (mlalamikaji) alikata rufaa ya madai dhidi ya walalamikiwa akidai kukashfiwa. Mgogoro ulitokana na kauli zilizodaiwa kutolewa na walalamikiwa ambazo mlalamikaji aliziona kuwa ni za kashfa. Hata hivyo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma ilitupilia mbali kesi ya mlalamikaji kwa maelezo kuwa maneno yaliyodaiwa kuwa ya kashfa yalikuwa ya kweli, na yalilenga kulinda masilahi ya kanisa.

Mlalamikaji alipinga uamuzi huo kwa hoja kuwa mahakama ya mwanzo haikuzingatia vipengele vyote vya msingi katika kesi ya kashfa, na pia kuwa mshtakiwa wa nne hakupata haki ya kusikilizwa. Mahakama Kuu ilibaini hoja kuu mbili: Mahakama ya Mwanzo ilishindwa kubainisha vipengele vyote vya kesi ya kashfa na kumnyima haki ya kusikilizwa mshtakiwa wa nne. Kwa msingi huo, Mahakama Kuu ilifuta mwenendo na hukumu ya mahakama ya mwanzo na kuamuru shauri lirudi kusikilizwa upya mbele ya hakimu mwingine mwenye mamlaka. Mbali na kusisitiza umuhimu wa haki ya kusikilizwa, Mahakama Kuu ilithibitisha kanuni zifuatazo za kisheria:

Mosi, ili mdai ashinde kesi ya kashfa, lazima athibitishe mambo matatu: kauli hiyo ilikuwa ya kashfa; ni lazima imsababishie madhara mlalamikaji; na ni lazima iwe ilichapishwa na mtu mwingine. Pili, ikiwa kauli hiyo itathibitika kuwa ni ya kweli, itakuwa ni utetezi dhidi ya kosa la kashfa. Utetezi mwingine ni pamoja na: kutoa maoni ya haki, upendeleo, kutokuwapo kwa nia ovu, na idhini ya mlalamikaji.

9 Rufaa ya Madai Na. 65 ya 2019 [2020] TZHC 1347.
10 Rufaa ya Madai Na. 31 ya 2022 [2023] TZHC 18371.




Photo by Andrew Medhat on Unsplash

# 2. Taratibu za kuanzisha kesi za jinai

## Nani anaweza kutoa malalamiko katika vyombo vya kutekeleza sheria kuhusu uchapishaji wa taarifa ya uongo inayokashfu, vitisho, kufedhehesha, au kupotosha umma?

Mtu yeyote (wa kisheria au wa asili) ambaye amekerwa na taarifa/kauli inayoweza kuharibu sifa zake anaweza kutoa malalamiko kwa polisi. Kesi inaweza kuripotiwa katika kituo cha polisi ambapo taarifa rasmi itaandikwa. Kisha, polisi watachunguza suala hilo ili kubaini kama kuna ushahidi wa kutosha. Iwapo ushahidi unaojitosheleza utapatikana, polisi wanaweza kumkamata mtuhumiwa na kuandaa hati ya mashtaka

baada ya kumhoji mhusika anayetuhumiwa kufanya kosa hilo (tazama Mwongozo wa Mashtaka ya Kesi za Jinai). Kisha, kesi hiyo itawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka wa Serikali (DPP) kwa ajili ya mapitio na kutoa uamuzi wa kushitaki au kutoshitaki. Endapo DPP ataona kuwa kuna ushahidi wa kutosha, kesi itaendelea mahakamani. Uamuzi wa kuendelea na mashtaka utategemea nguvu ya ushahidi, masilahi ya umma na vigezo vya kisheria.

## Ni nani anayeamua kuwa mwandishi wa habari ashtakiwe kwa kuchapisha taarifa ya uongo ambayo ina kashfa, vitisho, inafedhehesha, au kupotosha umma?

Makosa ya jinai hushtakiwa kwa niaba ya serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka wa Serikali. Katika kufanya uamuzi wa kumshtaki mtu au la, waendesha mashtaka huongozwa na Mwongozo wa Mashtaka ya Kesi za Jinai unapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.



REUTERS/Emmanuel Herman

# Je nifanye nini nikikamatwa na/au kushtakiwa kwa kuchapisha taarifa ya uongo inayoharibu sifa ya mtu, yenye vitisho, yenye kufedhehesha, au kupotosha umma?

Ukikamatwa na/au kushtakiwa, unapewa haki ya kufaidika na haki za mtu aliyekamatwa kama zinavyobainishwa katika Mwongozo wa Mashtaka ya Kesi za Jinai.

Ukiwa kizuizini una haki zifuatazo:

**(a)** kupewa taarifa kuhusu sababu ya kukamatwa (Hata hivyo, Mwongozo wa Mashtaka ya Kesi za Jinai unasema kuwa mtu aliyewekwa kizuizini anaweza asipewe sababu ya kukamatwa ikiwa "anasababisha sababu hiyo isitekelezeke kwa ofisa anayemkamata ili kumpa taarifa ya kosa hilo.");

**(b)** kupelekwa mahakamani haraka iwezekanavyo (ndani ya saa 24 baada ya kukamatwa) "isipokuwa kama kosa linaonekana kwa ofisa huyo kuwa ni kosa zito sana"[11];

**(c)** kufahamishwa kila kipengele cha kosa unaloshtakiwa nalo;

**(d)** unaposhtakiwa, hati ya mashtaka na maelezo yake yasomwe kwa lugha unayoifahamu au kuielewa;

**(e)** kupatiwa mkalimani iwapo huelewi lugha inayotumika mahakamani. Hii imeainishwa katika Kifungu cha 211 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai;

**(f)** kuachiliwa kwa dhamana au bila dhamana, kwa masharti ya kutoa kiasi cha fedha kuwa dhamana ya kuhudhuria mahakamani kwa tarehe na muda utakaoainishwa katika waraka wa dhamana[12]; na

**(g)** ukitiwa hatiani, una haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa mahakama ya awali au chombo cha usuluhishi.

11 Tazama Kifungu cha 32 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.
12 Vilevile.


REUTERS/Stringer

# Utaratibu wa kuanzisha kesi ya madai ya kashfa Tanzania

## Ni kwa namna gani mtu aliyelalamika anaweza kumfungulia mashtaka mwandishi/chombo cha habari kwa madai ya kashfa?

Mtu yeyote, awe wa kisheria (kama vile kampuni) au watu wa kawaida (mtu binafsi), anaweza kufungua mashtaka ya madai ya kashfa. Utaratibu wa kuanzisha kesi ya madai ya kashfa umeainishwa katika Kanuni za Huduma za Vyombo vya Habari (Mashauri ya Kashfa) za 2019.

Wanafamilia wanaweza kuendelea na madai ya haki kwa niaba ya marehemu iwapo uharibifu wa sifa yake umeendelea. Hata hivyo, watahitaji kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka wa Serikali ili kuanzisha kesi hiyo.[13] Hizi ni hatua ambazo mlalamikaji anaweza kufuata:

### Hatua ya 1: Mlalamikaji kuthibitisha kuwa kuna msingi wa kisheria wa kufungua kesi ya kashfa

### Hatua ya 2: Kuanzisha mashauri

Kesi ya madai ya kashfa inapaswa kufunguliwa kwa njia ya kutuma lalamiko kwa kutumia Kielelezo cha Fomu ya DP kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Huduma za Vyombo vya Habari (Mashauri ya Kashfa) za 2019.

### Hatua ya 3: Kuwasilisha waraka wa mashtaka ya kisheria

Mlalamikaji anapaswa kumpatia mdaiwa nakala ya malalamiko ndani ya siku 7 tangu kufungua kesi. Katika siku 7 baada ya kuwasilisha malalamiko, mlalamikaji anatakiwa kuwasilisha mahakamani kiapo kilichoandikwa na kuapwa, kikieleza majina, anuani ya sehemu na tarehe aliyokabidhi nakala ya malalamiko kwa watu wote wanaotuhumiwa kufanya kashfa.

### Hatua ya 4: Majibu ya mashtaka ya kisheria

Mdaiwa anapaswa kuwasilisha majibu ya malalamiko ndani ya siku 21 tangu kupokea madai. Iwapo mdaiwa atashindwa kuwasilisha majibu kwa muda huo na mahakama ikakataa ombi la kuongeza muda, mahakama itasikiliza kesi upande mmoja tu, kwa kutegemea ushahidi na nyaraka za mlalamikaji.

### Hatua ya 5: Uamuzi kuhusu mapingamizi ya awali

Mdaiwa anaweza kuwasilisha pingamizi la awali linalopinga mamlaka ya kisheria ya mahakama kusikiliza shauri hilo. Pingamizi hilo linapaswa kuwasilishwa wakati wa kuwasilisha majibu ya maombi. Mahakama inatakiwa kutoa uamuzi kuhusu pingamizi hilo ndani ya siku 30 baada ya pande zote kuwasilisha nyaraka zao.

### Hatua ya 6: Usikilizwaji wa kesi

Mahakama itapitia viapo vilivyowasilishwa na kusikiliza ushahidi kutoka kwa mashahidi. Baada ya usikilizwaji, mahakama inaweza kuruhusu pande zote mbili kutoa hoja kwa mdomo au kwa maandishi.

### Hatua ya 7: Hukumu

Mahakama inapaswa kutoa uamuzi wa kesi ndani ya miezi 6 tangu kukamilika kwa hatua za awali. Mahakama inaweza kuongeza muda wa kuamua kesi kwa miezi mingine mitatu ikiwa ni lazima.

13 Kifungu cha 35(3) cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016.

# Ni wapi mlalamikaji atafungua kesi ya madai ya kashfa?

Kesi ya madai ya kashfa inaweza kushughulikiwa kupitia njia mbalimbali kulingana na mahakama na mazingira maalumu ya kesi inayohusika. Njia zilizopo kwa upande wa mlalamikaji ni pamoja na Mahakama Kuu, Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya[14] na njia zingine mbadala za usuluhishi wa migogoro kama ifuatavyo:

## Mahakama za kisheria

Hizi ni:

(a) **Mahakama Kuu:** mahakama hii ina mamlaka ya kisheria kuhusiana na kesi kubwa za kashfa hasa ikiwa kesi inahusisha maswali magumu ya kisheria au madai makubwa ya fidia. Sheria haielezei thamani ya kifedha ya kesi ambayo mahakama kuu itasikiliza.

(b) **Mahakama ya Wilaya:** ina mamlaka ya kisheria kusikiliza kesi za madai na jinai katika wilaya husika, na vilevile, inashughulikia ukataji wa rufaa wa kesi na kupitia upya maamuzi ya Mahakama ya Mwanzo. Inaweza kushughulikia kesi ya jinai ya kashfa zisizozidi Tshs. 300,000,000.

(c) **Mahakama ya Hakimu Mkazi:** ina mamlaka ya kisheria katika eneo linalobainishwa na Amri ya Jaji Mkuu. Pia, inasikiliza kesi za kashfa zisizozidi Tshs. 300,000,000.

(d) **Madai Madogo:** ikiwa kiwango cha fidia kinachodaiwa ni chini ya TSh. 100,000,000, kesi ya kashfa inaweza kusikilizwa katika Mahakama ya Wilaya au ya Hakimu Mkazi kwa kutumia utaratibu wa mashauri madogo. Utaratibu huu huwa wa haraka zaidi, hauna urasmi na wakati mwingine pande hazihitaji kuwapo kwa wakili.

**Baraza Huru la Vyombo vya Habari:** Baraza hili lilianzishwa chini ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ili kushughulikia malalamiko kati ya vyombo vya habari na umma. Sheria inatoa fursa ya kuundwa kwa Kamati ya Malalamiko chini ya Baraza Huru la Vyombo vya Habari. Kamati ya Malalamiko inashughulikia malalamiko kuhusu maudhui yanayochapishwa na vyombo vya habari. Ikiwa mtu hataridhika na uamuzi wa Baraza, anaweza kukata rufaa katika Mahakama Kuu.

## Utatuzi mbadala wa migogoro (ADR)

**Usuluhishi:** Pande zinazohusika zinaweza kuamua kumaliza mgogoro wa kashfa kupitia usuluhishi, ambapo mtu wa kati asiyeegemea upande wowote huwasaidia kufikia makubaliano ya maridhiano bila kwenda mahakamani.

14 Kanuni ya 3 ya Kanuni za Huduma za Vyombo vya Habari (Mashauri ya Kashfa) za 2019.

# Nifanye nini endapo nimetumiwa hati ya mashtaka ya madai ya kashfa?

**Hatua ya 1: Tafuta msaada wa kisheria**

Mwombe wakili mwenye utaalamu katika masuala ya sheria za kashfa au sheria za vyombo vya habari ili akusaidie kujitetea ipasavyo.

**Hatua ya 2: Pitia kwa makini malalamiko**

Chunguza madai yaliyomo ili kubaini kauli au taarifa maalumu zinazodaiwa kuwa za kuchafua jina na tathmini uhalali wake.

**Hatua ya 3: Kusanya ushahidi**

Kusanya ushahidi wa kuunga mkono utetezi wako ili kupinga madai yaliyotolewa au kuanzisha utetezi kama uliopo hapa chini:

- vyanzo vya taarifa au chapisho lililolalamikiwa;
- tafuta nyaraka au rekodi zinazoonesha ukweli wa taarifa hiyo; na
- tafuta maelezo au tamko la uthibitisho kutoka kwa mashahidi.

**Hatua ya 4: Wasilisha majibu ya madai**

Andaa na wasilisha majibu ya madai ndani ya siku 21 tangu tarehe ya kupokea huduma hiyo. Majibu yanaweza kueleza hoja za utetezi kama vile ukweli, maoni ya haki au upendeleo, miongoni mwa mambo mengine. Pia, katika hatua hii unaweza kuweka pingamizi ikiwa mahakama haina mamlaka ya kisheria kusikiliza kesi hiyo.

**Hatua ya 5: Fikiria kufikia mwafaka/makubaliano**

Ikiwa madai yana msingi, tafakari kuhusu njia za kusuluhisha mgogoro nje ya mahakama, kama kufuta kauli au kuomba msamaha.

**Hatua ya 6: Jiandae kwa ajili ya usikilizwaji wa kesi**

Shirikiana kwa karibu na wakili wako ili kuandaa utetezi madhubuti, ikiwa ni pamoja na maandalizi ya mashahidi na hoja za kisheria.



SHUTTERSTOCK/Westock Productions

# 4. Utetezi dhidi ya madai ya kashfa

## Nawezaje kujitetea katika kesi ya kuharibu sifa ya mtu/kashfa?

Iwapo itathibitika kuwa mwandishi wa habari amechapisha taarifa yenye maneno ya kashfa, mwandishi huyo atawajibika kutoa utetezi wa kisheria unaoonesha sababu halali ya kuchapisha taarifa hiyo. Waandishi wa habari (Watuhumiwa) wa kesi ya kashfa wanaweza kutumia mojawapo ya hoja hizi kama utetezi ili kubatilisha kutiwa hatiani na sheria:

### Ukweli

Iwapo maneno ya kashfa yana ukweli na yalitolewa kwa "manufaa ya umma."[15]

15 Kifungu cha 37 cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016.

## Haki ya kinga kamili

Uchapishaji wa jambo la kashfa ni haki ya kinga kamili, na mwandishi wa habari hapaswi kuadhibiwa pale ambapo jambo lililochapishwa ni taarifa halali ya jambo lolote lililosemwa au lililofanyika au kutangazwa Bungeni.[16] Haidhuru kama taarifa hiyo ni ya uongo. Pia, haidhuru kama taarifa hiyo ilichapishwa kwa nia mbaya au kwa nia njema.

## Haki ya kinga ya masharti/kinga ya masharti maalumu

Kinga ya masharti hutumika pale ambapo taarifa imechapishwa kwa nia njema. Nchini Tanzania, hali hii hujumuisha taarifa ya haki kuhusu yaliyosemwa, yaliyofanywa au kuoneshwa katika mashauri ya madai au ya jinai au uendeshaji wa mashtaka kabla ya kwenda mahakama yoyote.[17] Utetezi huu utafeli ikiwa mahakama ilikuwa imepiga marufuku kuchapisha taarifa yoyote iliyotajwa au kuoneshwa mbele yake kabla kwa sababu ya uchochezi, maadili mabaya au kutukana dini. Pia, utetezi huu unajumuisha kuchapisha tena taarifa ambayo ilikwishachapishwa ambayo inanufaika na kinga ya masharti maalumu.

## Pendekezo la kurekebisha kosa na uchapishaji usio wa nia mbaya[18]

Mwandishi wa habari anayetambua makosa yake kwa kuchapisha taarifa ambayo ina tuhuma za kumkashifu mtu mwingine anaweza kufanya marekebisho kwa mtu aliyeathirika, ikiwa taarifa hiyo ilichapishwa kwa bahati mbaya. Ili kuonesha kuwa chapisho halikuwa la makusudi, marekebisho yatakayofanyika ni lazima yaambatishwe na hati ya kiapo kinachoeleza ukweli ambao mwandishi wa habari aliuegemea. Marekebisho yatakayofanyika yanajumuisha kutoa marekebisho ya taarifa, kuomba radhi, au kuwajulisha wale waliopewa nakala za chapisho kuwa taarifa hiyo inamkashifu mtu, ikiwa mlalamikaji hakubaliani na msamaha ulioombwa na mwandishi, basi mwandishi wa habari anaweza kuegemea katika utetezi wa kuwa amefanya marekebisho na kwamba hakuchapisha taarifa kwa nia mbaya.

16 Kifungu cha 38 cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016.
17 Kifungu cha 39 cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016.
18 Kifungu cha 40 cha Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya 2016.



Photo by Joshua Hoehne on Unsplash

# 5. Hatua za kivitendo za kupunguza uwajibikaji wa kisheria kutokana na kashfa

Waandishi wa habari Tanzania wanapaswa kuongozwa na Kanuni za Maadili ya Wanahabari zilizotolewa na Baraza la Vyombo vya Habari Tanzania. Pia wanapaswa kuongozwa na Kanuni za Huduma za Vyombo vya Habari (Marekebisho), na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni).

## Muhtasari

Ni muhimu kukumbuka kuwa ukweli ni utetezi kamili dhidi ya madai ya vitendo vya kashfa. Huenda kukawa na vizuizi vingine vya kuchapisha taarifa, lakini ilimradi taarifa hiyo ni ya kweli na inaweza kuthibitishwa kuwa ya kweli, madai ya uchafuaji jina hayawezi kufanikiwa. Kanuni nzuri ya kufuata ni kuripoti tu yale ambayo una uhakika unaweza kuyathibitisha.

Kuzingatia kwa makini usahihi na haki ya taarifa unayotoa, na kuthibitisha ukweli wa yaliyosemwa, kunaweza kukuweka katika nafasi nzuri iwapo utakumbana na vitisho au mashtaka ya kisheria. Mapendekezo yafuatayo hapa chini yanalenga kukusaidia wewe kufikiria kuhusu njia za kivitendo za kufanikisha jambo hilo. Pia, kuna utetezi mwingine dhidi ya mashtaka ya kashfa unaopatikana kwa ajili yako kutegemeana na mahakama husika. Baadhi ya utetezi huo ni huu hapa chini.

## Ukusanyaji wa taarifa

- Kusanya taarifa mapema – Kadiri muda unavyopita, kumbukumbu na vyanzo vya taarifa vinakuwa dhaifu au kupatikana kwa uchache.
- Tumia vyanzo vya siri kwa tahadhari – Ikiwa unategemea taarifa kutoka katika chanzo cha siri, kuhusiana na taarifa za madai fulani au maelezo katika utoaji wa taarifa, kuwa makini kwa sababu inaweza kuwa vigumu kuthibitisha madai ya ukweli.
- Makubaliano ya kutofichua taarifa yanakubalika na yanafaa kumlinda mwandishi wa habari kutofichua chanzo chao cha taarifa. Ikiwa hutafikia mapatano hayo – yawe yamebainishwa kabisa kwa maandishi au kwa vitendo, au hayajabainishwa - huwezi kulazimika kisheria (ingawa kimaadili unaweza) kulinda chanzo cha taarifa na kutunza siri.
- Tumia rekodi za umma kwa faida yako. Unaweza kuzitumia rekodi hizo kuthibitisha taarifa uliyoipata kutoka katika vyanzo vingine.
- Endapo utachagua kutumia rekodi za sauti au video, daima fikiria kama huhitaji kibali cha kurekodia, au kama utahitaji kibali cha kurekodia. Ukiwa na shaka, omba idhini.
- Tunza vizuri kumbukumbu za nyaraka , mikutano, n.k.
- Fanya utafiti wa kina. Thibitisha vyanzo vya taarifa kuwa ni sahihi na chunguza ukweli wa taarifa mara mbili. Kwa kawaida, unaweza kuchukua taarifa kutoka katika mamlaka mbalimbali au wakala wanaotambulika bila kuwa na uthibitisho wa ziada, ilimradi umetaja chanzo cha taarifa hiyo waziwazi.

## Kuandaa na kuhakiki makala

- Ifahamu sheria ya kashfa katika nchi unayofanyia kazi (tazama hapo juu). Kuwa makini katika baadhi ya nchi kuna sheria kali zaidi – kwa mfano, katika baadhi ya nchi ni rahisi kwa kampuni kufungua kesi ya kashfa kuliko watu binafsi.
- Fahamu na kubaliana na miongozo na sera za maadili ya taarifa ya shirika lako la habari.
- Tumia vyanzo vya taarifa vinavyoaminika ili kuthibitisha usahihi wa taarifa yoyote inayoweza kuwa na maneno ya kashfa.

- Jiulize ikiwa kuna kauli/maneno yoyote yanayomlenga mtu au kampuni yanayoweza kuharibu sifa yao. Thibitisha usahihi wake, na ikiwa kuna shaka iliyosalia, fikiria kwa makini uwezekano wa kutochapisha chapisho hilo.

- Tegemea zaidi vyanzo vya Habari vinavyoaminika na visivyo vya siri – kwa mfano, kwa kuwa na kiungo kuunganisha taarifa au vinginevyo vinavyofichua taarifa inayohusika au rekodi za umma.

- Misingi ya kuwajibika kwa mwandishi wa habari ni kutafuta maoni kutoka kwa wahusika wa taarifa uliyoikusudia kuichapisha – hasa ikiwa pale unapodhamiria kuanzisha madai dhidi yao au mwenendo wao – unapaswa kuweka chanzo cha madai hayo kwa uwazi kwa mhusika mapema na uwaombe majibu yao.

- Hakikisha hasa pale unapofanya uandishi wa habari wa kiuchunguzi, wahusika unaowatuhumu wana muda wa kutosha kujibu na wa kutoa taarifa na kutoa majibu yanayojitosheleza. Hupaswi kuwaonesha rasimu ya makala unayokusudia kuitolea taarifa, lakini unapaswa kujiandaa kushirikisha chanzo cha chapisho unalotarajia.

- Tafakari maoni/ majibu yao katika makala (Unaweza kutumia busara yako ya uhariri katika kufanya hayo). Hata kama hakuna mtu aliyeandika kitu chochote, "hakuna aliyetoa maoni" au "hakuna chanzo" kutadhihirisha kuwa ulifuata taratibu sahihi za kutoa taarifa za kweli.

- Tumia lugha sahihi kuelezea maana uliyoikusudia. Epuka utata, maneno ya uongo kupitiliza au kubahatisha. Kwa kadiri ambavyo umetumia dhana au umedhahania, weka wazi kuwa ni dhana.

- Daima hakikisha kuwa nukuu zinatumika kwa usahihi na taja chanzo cha nukuu hizo waziwazi.

- Zingatia kuondoa mazingira ya tuhuma na epuka utoaji wa taarifa zinazoegemea upande mmoja. Utoaji wa taarifa lazima uwe na uwiano na sio kupotosha uhalisia.

- Usieneze uvumi bila ushahidi uwe wa masula ya umma au jambo binafsi. Ripoti tu pale ambapo kuna msingi wa kutosha na useme wazi kile usichokijua.

- Zingatia namna wahusika wa habari yako walivyo hatarishi au wenye uzoefu wa kufungua mashtaka, na ujipange vya kutosha. Kama muhusika ni mtu mwenye historia ya kushtaki vyombo vya habari, ishirikishe timu ya kisheria ya taasisi yako.

- Tambua iwapo unafanya utetezi wa haki au maoni muhimu yaliyolindwa. Kunapaswa kuwapo na ushahidi wa kutosha kwa ajili ya ukweli wa maneno. Ikiwa kuna jambo lisiloeleweka au shaka yoyote, kumbuka kuelezea kama maelezo ya maoni (yenye msingi katika ukweli) au kuwasilisha kama dhana.

- Kuwa na tahadhari ya kuchapisha upya madai. Ikiwa utatumia taarifa kutoka chanzo kingine, utakuwa unawajibika nayo. Hakikisha umefanya utafiti wako binafsi.

- Zingatia iwapo utetezi wowote dhidi ya shtaka la kashfa unapatikana- kama vile ukweli, utoaji taarifa kwa masilahi ya umma, haki ya kinga kamili au ya masharti maalumu, taarifa sahihi na za haki za mwenendo wa jambo fulani.

- Kuna utetezi mwingi kuhusu kitendo cha kashfa zaidi kuliko ukweli /utekelezaji wa sheria, ambapo baadhi yake unaweza kuwa mahususi kwa matumizi ya waandishi wa habari – kwa mfano, katika baadhi ya nchi upo utetezi pale ambapo makala inaelezea maoni yaliyoandikwa kwa masilahi ya umma. Hata hivyo, utetezi huu si wa uhakika kabisa na kwa kawaida utahitaji kutimiza masharti kadhaa. Ikiwa unatarajia kutumia utetezi huu, wasiliana na timu yako ya kisheria au fanya utafiti wa kesi zilizopita.

# Baada ya kuchapishwa

- Endelea kufuatilia maendeleo yoyote kuhusu jambo lililoripotiwa ambalo linaweza kubadilika, kuhoji au kutoa mwanga mpya kuhusu taarifa zilizochapishwa. Ripoti zilizoruhusiwa awali kwa ujumla zinaweza kuhifadhiwa katika kumbukumbu za mtandaoni. Kwa kawaida huna jukumu la kuchunguza au kuhuisha taarifa hizo.

- Ikiwa upande ulioathirika utatoa malalamiko yenye msingi, huenda ukahitajika kuongeza taarifa za ziada au kuchukua tahadhari za msingi ili kuzuia taarifa hizo zisipatikane katika visakuzi kwa jina linalohusiana na utafutaji wa maelezo ("haki ya kusahaulika").

- Fikiria kuhusu kuhifadhi nukuu zako na mawasiliano muhimu, na ikiwa ni hivyo, kwa muda gani – kufahamu ukomo wa muda wa kuwasilisha madai ya kukashfiwa katika eneo linalohusika la utekelezaji wa masuala ya kisheria linaweza kusaidia.

- Kuwa tayari kusahihisha au kuondoa makosa yako na kuomba msamaha kwa kiwango kinachohitajika kwa ajili ya utetezi wa ukweli kisheria. Huenda ukahitajika kusahihisha madai ya kweli ambayo baadaye yameoneshwa kuwa si sahihi na yana athari ya kudumu kwa haki za mtu anayehusika. Hii kawaida hufanywa kupitia masahihisho ya nyongeza katika toleo lijalo au kwenye tovuti.

*Tafadhali kumbuka kuwa, waandishi wa habari wanapaswa pia kuwa makini na mwelekeo mpya katika maeneo mengine ya sheria ambayo yanaweza kuathiri ustawi wao au kuleta hatari za kisheria - kama vile sheria za faragha zinazotumika.*

## Kuhusu Thomson Reuters Foundation

Thomson Reuters Foundation ni taasisi iliyoasisiwa na Thomson Reuters, kampuni inayoongoza duniani katika masuala ya huduma za habari na teknolojia. Kama taasisi huru ya kutoa misaada, iliyosajiliwa Uingereza na Marekani, tunatumia utaalamu wetu wa vyombo vya habari, sheria na data ili kuimarisha uandishi huru wa habari, kuwezesha ufikiaji wa sheria na kukuza uwajibikaji katika biashara. Kupitia habari, maendeleo ya tasnia ya habari, msaada wa kisheria bila malipo na maarifa ya data, tunalenga kujenga jamii huru, za haki na zenye maarifa.

TrustLaw, ni mradi wa Thomson Reuters Foundation, mtandao mkubwa zaidi duniani wa msaada wa kisheria wa bure. Kwa kufanya kazi na makumpuni yanayoongoza ya sheria na timu za kisheria za mashirika, tunatoa msaada wa kisheria, tafiti za kisheria zenye matokeo makubwa na nyenzo kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo huru vya habari na biashara za kijamii katika nchi zaidi ya 190. Kwa kusambaza utamaduni wa kutoa msaada wa kisheria wa bure, TrustLaw inalenga kuimarisha jamii ya kiraia na kuchochea mabadiliko chanya. Ikiwa una mawazo yoyote au nyenzo tunazoweza kutengeneza au miradi ya utafiti wa kisheria yenye uwezo wa kuwa na msaada baada ya kusoma muongozo huu, tafadhali wasiliana nasi. Ikiwa wewe ni shirika lisilo la kiserikali au biashara ya kijamii unayehitaji msaada wa kisheria, unaweza kupata taarifa zaidi kuhusu huduma zetu hapa na kujiunga na TrustLaw bila malipo.

## Kuhusu iWatch Africa

iWatch Africa ni shirika lisilo la kiserikali la vyombo vya habari na masuala ya sera lenye hadhi ya ushawishi mkubwa kitaifa. Shirika hili limejijengea nafasi muhimu katika mazingira ya sera na uandishi wa habari nchini Ghana kwa kutoa tathmini huru, ya ukweli na inayotegemea ushahidi kuhusu masuala mbalimbali.

iWatch Africa hufuatilia haki za kidijitali barani Afrika, uhalifu uliopangwa unaovuka mipaka, ukiukwaji wa haki za binadamu, mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa bahari na utendaji wa serikali kwa ujumla nchini Ghana.

Kupitia matumizi ya uandishi wa habari wa takwimu, simulizi na utetezi wa sera, iWatch Africa inaunda mjadala wa kitaifa na kikanda ili kuimarisha uwazi, uwajibikaji na ushiriki wa wananchi katika utawala barani Afrika.

# Shukrani na Kanusho

Thomson Reuters Foundation na iWatch Africa wanapenda kutoa shukrani kwa timu ya kisheria ya Ideal Law Group, waliotumia muda na utaalamu wao bila malipo kufanikisha uandaaji wa Mwongozo huu. Mwongozo huu umetolewa kwa madhumuni ya taarifa pekee. Haukusudii kuwa ushauri wa kisheria. Wasomaji wanahimizwa kutafuta ushauri kutoka kwa wanasheria waliofuzu kulingana na hali zao binafsi. Licha ya jitihada za kuhakikisha usahihi na uhalali wa taarifa zilizomo wakati wa kuchapishwa, hatuhakikishi ukamilifu wake, hasa ikizingatiwa kuwa hali zinaweza kubadilika baada ya kuchapishwa. Ideal Law Group na Thomson Reuters Foundation hawatakuwa na dhima au wajibu wowote kwa hatua zilizochukuliwa au kutokuchukuliwa wala kwa hasara yoyote inayotokana na kutegemea Mwongozo huu au makosa yaliyomo ndani yake.



Photo by Emediong Umoh on Unsplash

TrustLaw, mradi wa Thomson Reuters Foundation, ni mtandao mkubwa zaidi duniani wa msaada wa kisheria wa bure. Kwa kufanya kazi na makumpuni yanayoongoza ya sheria na timu za kisheria za mashirika, tunatoa msaada wa kisheria, tafiti za kisheria zenye matokeo makubwa na nyenzo kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo huru vya habari na biashara za kijamii katika nchi zaidi ya 190.

Kwa maelezo zaidi, tembelea www.trust.org.

TrustLaw | Thomson Reuters Foundation